SPIRITUALGIFTSTEST.com

# MTIHANI WA KARAMA ZA KIROHO KWA VIJANA

**Maagizo:**

Warumi 12:3 inasema, "Kutokana na neema aliyonijalia Mungu, nawaambieni nyinyi nyote: Msijione kuwa ni kitu zaidi kuliko mnavyopaswa kuwa. Fikira zenu na ziwe na kiasi kadiri ya kipimo cha imani Mungu aliyomgawia kila mmoja."

Ili kupata matokeo bora zaidi, jibu kila kauli kulingana na sifa ulizonazo, sio sifa ambazo ungetaka kuwa nazo ama unazofikiria unastahili kuwa nazo. Je, kauli hizi ni za ukweli kwa kiwango gani? Je, uzoefu wako umekuwa upi? Je, watu wengine wanakuambia nini? Je, kauli hizi zinaashiria jinsi unavyoyaishi maisha yako ya kila siku kwa kiasi gani? Kila swali ni muhimu, kwa hivyo jaribu kujibu maswali yote. Utahesabu alama utakazopata mwishoni mwa mtihani.

**Jibu kila kauli kulingana na kipimio cha pointi 1-5 kifuatacho:**
**1 = Sio Sahihi Kabisa**
**2 = Sio Sahihi Kwa Kiasi**
**3 = Sio Sahihi Wala Sahihi**
**4 = Sahihi Kwa Kiasi**
**5 = Sahihi Kabisa**

---

**Anza:**

1. _____ Ninaweza kuwapanga marafiki zangu au wanafunzi wenzangu ili kutimiza lengo au kazi.
2. _____ Ninataka kuanzisha makanisa na/au huduma mpya.
3. _____ Ninaweza kujua kama kauli imetolewa kwenye Biblia au la.
4. _____ Nina ufahamu mzuri wa injili na ninaweza kuwaelezea wengine kwa urahisi.
5. _____ Ninawahamasisha watu wengine wanaopitia wakati mgumu katika imani yao.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

6. _____ Nina imani kubwa kuwa Mungu binafsi anajihusisha na maisha yangu kwa undani.
7. _____ Situmii pesa zangu kwa vitu nisivyovihitaji ili niweze kumtolea Mungu zaidi.
8. _____ Watu huniuliza ufafanuzi wangu wa mistari hususa ya Biblia.
9. _____ Watu wengine hufuata uongozi wangu.
10. _____ Ninawahurumia wale wanaopitia mambo magumu katika maisha yao.
11. _____ Ninaombea watu wengine.
12. _____ Mungu amenipa ujumbe kwa mtu binafsi au kundi la watu na kunihimiza niwafikishie ujumbe huo.
13. _____ Ninafurahi kufanya majukumu ya kila siku yanayosaidia huduma tofautitofauti kanisani.
14. _____ Ninatumia muda mwingi kusoma Biblia ili niweze kuleta mabadiliko katika maisha ya watu.
15. _____ Nina maarifa yenye msaada wakati wa mambo magumu.
16. _____ Ninaweza kutengeneza mpango kwa urahisi na kuuweka mahali pake ili kukamilisha jambo.
17. _____ Ninafanya kazi vizuri na watu wanaotoka kwenye mandharinyuma tofautitofauti.
18. _____ Ninasikiliza kwa makini maneno ambayo watu wanasema na kufunza ili nione kama ni kweli au la.
19. _____ Moyo wangu ni mzito kwa wale waliopotea bila Yesu.
20. _____ Ninapoona mtu ambaye amevunjika moyo, ninamkumbusha kuhusu jinsi Mungu alivyo mkuu na kiasi alichoahidi atawatunza.
21. _____ Ninaamini Mungu atajibu maombi yangu kulingana na mapenzi yake makamilifu.
22. _____ Ninapenda kutoa pesa za kusaidia kanisa kueneza Injili.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

23. _____ Roho Mtakatifu amenipa ujumbe ambao nimeutumia kusaidia wengine.

24. _____ Ninapenda kuweka miradi na kuitimiza, hata kama watu wengine wataipinga.

25. _____ Ninawaona wagonjwa na maskini kama watu wanaohitaji zaidi upendo na faraja Yesu anazotupa.

26. _____ Ninapenda kuwasaidia wengine kujifunza na kukua katika imani yao.

27. _____ Nimepokea ujumbe kutoka kwa Mungu na nikawaambia watu kanisani.

28. _____ Ninajitolea kwa furaha kusaidia kanisani ninapojua itatimiza haja fulani.

29. _____ Ninapotoa mafunzo ya Biblia, wengine hupendezwa na kutaka kujifunza zaidi.

30. _____ Ninautumia uzoefu wangu wa maisha kusaidia watu wengine wanaopitia shida ambazo nimewahi kuzipitia.

31. _____ Wakati nikiwa kwa kikundi, huwa ninaona kwa uwazi jinsi ambayo kila mtu anaweza kuchangia ili tutimize mradi wetu pamoja.

32. _____ Ninahudumia watu wa tamaduni tofauti vizuri.

33. _____ Ninaweza kugundua kwa urahisi kama mtu ni mwongo au bandia.

34. _____ Kila mara ninatafuta nafasi za kujenga uhusiano na watu wasio Wakristo.

35. _____ Ninahisi Mungu akinisukuma niwahamasishe wale ambao hawakui katika imani.

36. _____ Ninajua Mungu atanisaidia hata kama sioni jinsi atakavyonisaidia.

37. _____ Ninafurahi kujua kwamba ninapotoa kanisani watu watasaidika na wataambiwa kuhusu Yesu.

38. _____ Ninasoma Biblia ili niweze kuwaambia wengine ukweli wa Biblia.

39. _____ Siogopi kuchukua tahadhari ili kuendeleza ufalme wa Mungu.

40. _____ Ninajali sana kuhusu watu wanaoumia na ninataka kuwasaidia katika wakati wao mgumu.

41. _____ Uhusiano ni muhimu sana kwangu. Kwa hakika mimi ni "mtu wa watu."

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

42. _____ Mungu amenipatia taarifa kuhusu mtu ili ni nimkabili na kumrudisha kwa Mungu.

43. _____ Ninapenda kuwa kwenye mandharinyuma na sina haja ya kutambulika ninapohudumu kanisani.

44. _____ Ninafurahi kueleza vitu kwa watu ili waweze kukua kiroho na kibinafsi.

45. _____ Ninasaidia watu kwa kuwapa suluhisho za kibiblia za matatizo ya maisha.

46. _____ Ninapanga vitu ili maisha yangu yaende kwa urahisi zaidi.

47. _____ Mimi ni kiongozi mwenye ushawishi mkubwa.

48. _____ Ninaweza kuamua kwa upesi ikiwa kuna mvuto wa uovu katika hali fulani.

49. _____ Ninakaliri mistari ya Biblia ili kushiriki na wale wasiomjua Yesu kama Mwokozi wao.

50. _____ Mimi siogopi kutoa changamoto kwa mtu ikiwa najua itahamasisha ukuzi wao wa kiroho na ujasiri katika maisha yao.

51. _____ Nitajitokeza kwa ujasiri wa imani ninapoona kuwa Mungu ananiambia nifanye jambo fulani.

52. _____ Hata kama huwa natoa kiwango kizuri cha vitu nilivyonavyo kwa Mungu, huwa bado ananibariki na zaidi ya ninayohitaji.

53. _____ Ninakumbuka mengi ya yale ninayojifunza na nina kumbukumbu nzuri.

54. _____ Ninapenda kusaidia watu wengine kukua katika vipaji na uwezo wao.

55. _____ Ninapenda kusaidia watu wanapopitia magumu ya maisha na kuwaonyesha huruma aliyoonyesha Yesu.

56. _____ Ninajali kuhusu kanisa na ninataka kuiona ikikua na kujengwa kwa upendo.

57. _____ Mungu ameweka katika mawazo yangu mambo muhimu ambayo awali hayakujulikana ambayo nimetangaza kanisani.

58. _____ Ninaweka kando muda na kujitahidi kusaidia wale wanaohitaji msaada karibu nami.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

59. _____ Ninachukia wakati mtu anatumia mistari ya Biblia nje ya muktadha kwa haja za kibinafsi.

60. _____ Ninaweza kuona mahali ambako maamuzi ya mtu binafsi au kundi yatawaelekeza, na ninajitolea kuwaelekeza katika njia inayofaa.

61. _____ Ninajali kuhusu mambo yale madogo-madogo wakati ninapofanyia kazi kitu fulani.

62. _____Nimehitimu na ninaweza kuanzisha na kuongoza huduma mpya.

63. _____ Ninaweza kujua ikiwa mtu anakuwa mwongo kabla ya mtu mwingine yeyote.

64. _____ Ninashuhudia kuhusu yale Kristo aliyoyafanya katika maisha yangu na jinsi alivyo nisaidia.

65. _____ Watu wengine wameniambia kuwa maneno yangu ya kuwatia moyo yamesaidia kukua katika imani.

66. _____ Hata wakati wa magumu, ninaamini kuwa Mungu atanituliza na kunipa mahitaji yangu.

67. _____ Ninataka kufurahisha Mungu na jinsi ninavyotumia pesa zangu.

68. _____ Ninapenda kushiriki na watu wengine ukweli ambao Mungu amenionyesha.

69. _____ Watu hunitegemea kuongoza kikundi au mradi shuleni au kanisani.

70. _____ Ninajulikana kwa "kujali sana" na kusaidia watu wengine wanapohitaji usaidizi.

71. _____ Ninataka kuona kila mtu kanisani akitimiza kazi kubwa aliyokabidhiwa.

72. _____ Nimepokea kwa ghafla ujumbe wa kanisa letu kutoka kwa Mungu na nikawaeleza.

73. _____ Ninapoona hitaji kanisani, ninalikidhi bila kuulizwa.

74. _____ Nina sikiliza kwa makini maneno ambayo watu hutumia kwa sababu kila neno ni muhimu na lina maana.

75. _____ Huwa ninaelekeza watu kwenye Biblia wanapouliza ushauri wangu.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

76. _____ Ninajua jinsi ya kupanga wakati wangu ili kukamilisha kazi zangu za kila siku.

77. _____ Ninasaidia kufundisha viongozi wapya walio karibu nami.

78. _____ Nina "rada" yenye nguvu ya kugundua mafunzo ya uongo.

79. _____ Ninahisi kuwa ni lazima ni waeleze marafiki zangu kunhusu Yesu, hasaa wale wasioenda kanisani.

80. _____ Wakati watu wengine wanakabiliwa na matatizo magumu, ninawaliwaza kwa ujasiri kuhusu uaminifu wa Mungu kwa watu wake.

81. _____ Sina wasiwasi kwa sababu ninajua Mungu ana nguvu na atanisaidia katika kila shida.

82. _____ Ninatafuta njia ambazo mimi mwenyewe ninaweza kuwasaidia maskini na wasiojiweza.

83. _____ Ninaweza kuona jinsi ambayo injili inalingana na kila kipengee cha maisha.

84. _____ Siogopi kujitokeza na kushika usukani katika hali ngumu.

85. _____ Ninatafuta wale ambao "wametegwa" na kuwasaidia kuendeleza maisha.

86. _____ Injili ya Yesu Kristo ndicho kitu muhimu zaidi katika maisha yangu na huduma.

87. _____ Watu wengine wamesema kuwa Mungu amewazungumzia kwa uwazi na moja kwa moja kupitia ujumbe nilioshiriki nao.

88. _____ Ninaamini kuna umuhimu wa milele katika kufanya kazi za kawaida kanisani.

89. _____ Ninaposoma Biblia, kila mara huwa ninagundua mambo mapya na ya kuvutia kuhusu Injili.

90. _____ Ninaweza kuona kwa urahisi mpango au mbinu iliyo bora zaidi.

91. _____ Chumba changu huwa safi na kilichopangwa kila mara.

92. _____ Viongozi wengine huja kwangu niwape usaidizi na mwongozo.

93. _____ Watu wengine wameniambia kuwa mimi nihakimu mzuri wa tabia.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

94. _____ Mengi ya mazungumzo yangu na watu wasio Wakristo huniongoza kuzungumza kuhusu imani yangu katika Yesu.

95. _____ Ninapoona watu wakijikwaza kwenye imani yao, huwa ninawahimiza kuyakumbuka mambo ambayo Mungu ameyafanya na kurudi kwenye furaha anayowapa.

96. _____ Huwa ninawahimiza watu wengine kumwamini Mungu katika kila jambo.

97. _____ Ninapopata mshahara au posho, kitu cha kwanza ninachokifanya ni kuuliza Mungu angetaka nipeane.

98. _____ Ninaweza kukuimbuka mistari ya Biblia ili kuwasaidia watu walio katika hali yoyote.

99. _____ Huwa nina kaza fikira zaidi kwenye mambo madogomadogo.

100. _____ Watu wengine wamesema kuwa nimewatuliza katika wakati walio kuwa chini maishani mwao.

101. _____ Huwa ninasaidia watu wengine wawe kama Yesu.

102. _____ Ninaweza kukumbuka mara ambazo Mungu alinipa ujumbe hususa kwa Kanisa lake kupitia mimi.

103. _____ Ninapata furaha kuwa msaidizi na kusaidia wengine katika huduma zinginezo.

104. _____Roho mtakatifu hunipa maneno yafaao ya kusema wakati ninapofundisha kitu.

105. _____ Nina suluhisho za kibiblia kwa hali zinazochanganya au ngumu.

## Maelezo Ya Kupata Alama:

ANdika alama zako (kutoka 1-5) za kila swali kwenye sanduku lenye nambari ya swali hilo. Jumlisha kila safu na uandike alama zako za jumla juu ya ishara ya karama mwafaka. Baada ya kufanya hivyo, unaweza kuangalia ufungu ufuatao ili uone ni karama gani ya kiroho inayosiamamiwa na kila ishara. **Alama ya juu zaidi ya karama yoyote ni 35**. Jinsi alama ilivyo juu, ndivyo ulivyo imarika

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

katika karama hiyo ya kiroho kulingana na majibu yako. Alama ya **29 au zaidi** katika karama yoyote ni isara yenye nguvu ya kuwepo kwa karama hiyo katika maisha yako. Alama za kati ya **22 na 28** zinaweza kuashiria karama ya kiroho iliyo kwenye hatua ya "mche", hasaa ikiwa mojawapo au zaidi ya alama zako tatu za juu zaidi zipo kwenye ukakaya huu.

## Matriki ya Alama:

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| | 31 | 32 | 33 | 34 | 35 | 36 | 37 | 38 | 39 | 40 | 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
| | 46 | 47 | 48 | 49 | 50 | 51 | 52 | 53 | 54 | 55 | 56 | 57 | 58 | 59 | 60 |
| | 61 | 62 | 63 | 64 | 65 | 66 | 67 | 68 | 69 | 70 | 71 | 72 | 73 | 74 | 75 |
| | 76 | 77 | 78 | 79 | 80 | 81 | 82 | 83 | 84 | 85 | 86 | 87 | 88 | 89 | 90 |
| | 91 | 92 | 93 | 94 | 95 | 96 | 97 | 98 | 99 | 100 | 101 | 102 | 103 | 104 | 105 |
| **Jumla ya Alama** | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Ishara za Karama** | **Ad** | **Ap** | **Di** | **Ev** | **Ex** | **Fa** | **Gi** | **Kn** | **Le** | **Me** | **Pa** | **Pr** | **Se** | **Te** | **Wi** |

## Ishara za Karama:

**Ad** = Usimamizi

**Ap =** Utume

**Di** = Hekima

**Ev** = Uinjilisti

**Ex** = Kuhimiza

**Fa** = Imani

**Gi** = Kupeana

**Kn** = Maarifa

**Le** = Uongozi

**Me** = Huruma

**Pa** = Mchungaji

**Pr** = Kutabiri

**Se** = Huduma

**Te** = Kufundisha

**Wi** = Busara

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.